**PROGRAMU YA UKUZAJI UCHUMI JUMUISHI ZANZIBAR (BOOSTING INCLUSIVE GROWTH FOR ZANZIBAR, BIG-Z)**

## 1.0 UTANGULIZI

Programu ya Ukuzaji Uchumi Jumuishi Zanzibar inafadhiliwa na Benki ya Dunia. Programu hii iliidhinishwa rasmi tarehe 10 Juni 2021 na kusainiwa tarehe 19 Agosti 2021 baina ya Benki ya Dunia na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Programu hii ilianza rasmi utekelezaji wake tarehe 2 Disemba 2022 na imepangwa kutekelezwa kwa muda wa miaka mitano hadi Juni/Julai 2026/2027 kwa gharama ya Dola za Kimarekani milioni 150 ambazo ni mkopo kutoka benki ya Dunia.

Lengo kuu la program ni kuimarisha hali ya maisha ya wananchi na kukuza maendeleo ya kiuchumi katika maeneo ya Unguja na Pemba. Programu inakusudia kuimarisha miundombinu na utoaji wa huduma kwa jamii, uhifadhi na Usimamizi Jumuishi wa Mji wa Zanzibar. Program hii ina sehemu kuu tatu (3) kama zifuatazo:

a) Maendeleo ya Mijini na Miundombinu Jumuishi
b) Uimarishaji wa Taasisi kwa Uendeshaji wa Miji na Kuhamasisha Uvumbuzi
c) Uendelezaji wa Mradi, Ufuatiliaji na Tathmini

**SEHEMU YA KWANZA: Maendeleo ya Mjini na Miundombinu Jumuishi (Area-Besed Integrated Urban and Infrastructure Development)**

Sehemu hii itagharamia uwekezaji wa Miradi ya Miundombinu ya barabara za ndani na mitaro ya maji ya mvua ili kukabiliana na changamoto za kimaendeleo na huduma za misingi pamoja na kuimarisha Maisha ya wakaazi katika aina tatu za maeneo ya Zanzibar ambayo ni Mjini hasa (Urban Core), maeneo ya mjini yanayokuwa kwa haraka (Fast - Growing Urban Areas) na miji na Vijiji vinavyokua kwa kasi (Emerging Towns and Villages). Miradi itakayotekelezwa katika sehemu hii ni kama ifuatavyo:

i. **Mradi wa kuendeleza Eneo la Michenzani na Mradi Salama wa watembea kwa Miguu Mji Mkongwe (Integrated Mobility and Urban Upgrade Program for Zanzibar Metropolitan Center)**

Lengo kuu la, Mradi huu ni kuboresha Mazingira ya maeneo ya Michenzani kwa kuyafanya rafiki na salama kwa watembeaji kwa miguu na wafanya biashara. Mradi huu unakusudia kuendeleza upya eneo la michenzani (Michenzani Area Integrated Redevelopment Plan), kuchochea mabadiliko ya mwenedno wa usafiri, na kugeuza eneo la Mjini lililotawaliwa na vyombo vya moto vilivyosangamana mjini kuwa sehemu salama na Rafiki kwa watembea kwa miguu, na mahali pazuri pa kuishi na kufika kwa urahisi. Mradi unakusudia kuboresha mwenendo wa usafiri wa vyombo vya moto ambapo

inajumuisha ufuatiliaji wa barabara kuu za eneo la Michenzani na kuboresha njia za watembe kwa miguu, kuimarisha miundombinu ya Umeme, Miundombinu ya Maji taka, na kuboresha huduma za Jamii ikiwemo kuboresha maeneo ya wazi.

Pia mradi utajumuisha uandaaji wa sera na sharia za udhibiti wa usafiri wa umma kwa kukuza usalama wa ndani na maeneo ya karibu ya Mji Mkongwe.

**ii. Mradi wa Kuyapa hadhi Maeneo ya Mjini yanayokuwa kwa haraka Unguja (Area – Based Upgrading Investments for Unguja (AUI-U)**

Mradi huu unakusudia kuimarisha hali ya maisha ya wakaazi wa maeneo ya Mjini yanayokua kwa kasi yaliyo jirani na mji wa Zanzibar ambayo bado yanakabiliwa na changamoto za kukosa huduma za msingi kama ilivyo maeneo mengine ya mjini.

Mradi utashughulikia utatuzi wa changamoto mbali mbali katika maeneo ya Tomondo, Sebleni, Meya na Magomeni. Lengo kubwa ni kuyapa hadhi na kuyakuza maeneo haya kwa kujenga na kukarabati njia za ndani, kujenga mitaro ya maji ya mvua na kuweka taa za barabarani pamoja na kuimarisha maeneo ya wazi.

**iii. Mradi wa Kujenga uwezo wa Kudhibiti Taka Ngumu (Solid Waste Management Improvement Technical Assistance)**

Mradi huu una lengo la kuzijengea uwezo Mamlaka za Serikali za Mitaa (Mabaraza ya Manispaa, Halmashauri za Wilaya na Mabaraza ya Miji) Unguja na Pemba katika usimamizi wa taka ngumu.

**iv. Mradi wa Kuimarisha Vijiji Vinavyokua kwa Kasi Unguja- Nungwi, Chwaka na Makunduchi (Integrated Upgranding of Gateway Villages in Unguja)**

Mradi wa kuimarisha Vijiji vinavyokua kwa kasi Unguja unakusudia kuimarisha vijiji vinavyokua kwa kasi Unguja katika maeneo hayo. Mradi utasaidia kuboresha miundombinu ya Miji na vijiji vilivyoteuliwa ambavyo kwa sasa vinaonekana viko nyuma katika ukuaji wa uchumi na kukabiliwa na hali ya umasikini. Mradi huu utasaidia kuimarisha upatikanaji wa miundombinu ya Barabara za ndani, pamoja na ujenzi na ukarabati wa masoko. Uwekezaji huu utasaidia kuongeza upatikanaji wa masoko kwa wafanyabiashara wadogo wadogo wanaojidhughulisha na kazi za utalii na kuimarisha muingiliano mzuri kati ya wateja, watalii na jamii husika.

**v. Mradi wa Kuimarisha Miji ya Pemba - Chake chake, Mkoani, Wete na Micheweni (Area-Based Upgrading Investments for Pemba)**

Katika juhudi za kuweka usawa na kukuza haiba ya miji yetu, kuimarisha maisha ya wananchi, mradi utaendeleza maeneo mbali mbali ya miji kisiwani

Pemba. Mradi utasaidia kuimarisha upatikanaji wa Miundombinu ya Barabara za ndani, ujenzi wa Masoko, na Vituo vya daladala (Bus Terminals). Mradi unalenga kwenye kuimarisha huduma za kijamii na kutatua changamoto za miji ya Wete, Chakechake, Mkoani na Micheweni.

**SEHEMU YA PILI: kuzijengea Uwezo Taasisi za Serikali katika Usimamizi wa Miji na Kushajiisha Ubunifu (Strengthening Institutions for Urban Management and Encouraging Innovation)**

Sehemu hii inakusudia kugharamia kazi za kuimarisha uwezo wa taasisi za Serikali juu ya utunzaji na usimamizi wa miji na kushajiisha matumizi ya Teknolojia na ubunifu katika kutekeleza majukumu yao. Katika kufanikisha lengo la Mradi, sehemu hii itatekeleza kazi zifuatazo:

**i. Kuimaraisha Taasisi na Matumizi ya Teknologia (Institutional Strengthening and Use of Technology in Governance)**

Mradi wa BIG-Z unakusudia kuimarisha matumizi ya TEHAMA kwa lengo la kuboresha ukusanyaji na usimamiaji wa mapato yatokanayo na vyanzo mbali mbali katika Mabaraza ya Manispaa na Mabaraza ya Miji Unguja na Pemba.

**ii. Kuzijengea uwezo taasisi za Serikali**

Mradi umepanga kuzijengea uwezo taasisi za Serikali zinazohusika na utekelezaji wa kazi mbali mbali za Mradi ili kuziwezesha taasisi hizo kuwa na uwezo mzuri wa kusimamia Miradi itakayotekelezwa katika taasisi zao ikiwemo ununuzi wa vitendea kazi na mafunzo ya muda mfupi kwa baadhi ya wafanyakazi.

Programu ya BIG-Z pia inakusudia kuijenga uwezo Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) kwa kununua vifaa na mitambo ya kupimia vifaa vya ujenzi vinavyoingia Zanzibar *(Building Material Testing Equipment).* Aidha, Programu imepanga kutayarisha Mpango wa Maendeleo wa Kisiwa cha Pemba (Pemba Development Master Plan).

**SEHEMU YA TATU: Usimamizi na Uendeshaji wa Mradi (Project Management, Monitoring and Evaluation)**

Sehemu hii inahusu usimamizi wa shughuli zote za mradi ikiwa ni pamoja na usimamizi wa fedha, usimamizi wa mazingira na kijamii, ununuzi, ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mradi. Aidha, sehemu hii inawahudumia Washauri Elekezi wanaoajiriwa kwa ajili ya kusaidia uendeshaji wa mradi.